# OFISI YA WAZIRI MKUU

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## SHULE YA SEKONDARI YA WAVULANA SIMIYU

**Simu**
**0787 353 080**

S.L.P 526,
**BARIADI.**

**Simu**: MKUU WA SHULE: 0787353080

MAKAMU MKUU WA SHULE: 0610905502 / 0656180969

**Tarehe** …………

**NAMBA YA USAJILI WA SHULE:** S.6981
**NAMBA YA KITUO CHA MTIHANI:** S7676

**Mzazi/ Mlezi wa Mwanafunzi** ______________________________________________

**S.L.P** ____________________________________________

____________________________________________

**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WAVULANA SIMIYU KWA WANAFUNZI WA KIDATO CHA…………..**

**1. UTANGULIZI.**

Mwanafunzi tajwa hapo juu amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule hii kwa mwaka………..

**HONGERA SANA**

Shule ya Sekondari ya Wavulana Simiyu (**Simiyu Boys Secondary School**) ni ya bweni inayopatikana katika mkoa wa Simiyu ndani ya Halmashauri ya mji wa Bariadi katika mtaa wa Shimbale kata ya Mhango umbali wa kilomita 20 kutoka Bariadi mjini magharibi mwa mzunguko (round about) barabara inayoelekea Ngulyati au umbali wa kilomita 56 kutoka wilaya ya Magu kupitia barabara ya Ngulyati kutokea Mwanza.

Muhula wa masomo utaanza tarehe………………..hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe iliyotangazwa na serikali kwa ajili ya kuanza masomo na mwisho wa kuripoti ni siku kumi na nne (14) baada shule kufunguliwa saa 10:00 jioni.

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA: -

### 2.1 *Sare ya shule.*

a) Sare ya shule hii ni shati mbili (2) nyeupe za tetron mikono mirefu (long sleeve), suruali **NNE** (4), Mbili (2) rangi nyeusi na mbili (2) rangi ya kijivu kwa ajili ya kushindia. (**Suruali chini ukubwa inch 16)**

b) Sare za michezo kwa shule hii ni bukta na T-shirt za rangi ya blue pamoja na raba

c) Tai ndefu nyeusi

d) Sweta moja (1) rangi ya dark blue

e) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na Kamba vyenye visigino vifupi.

f) Fulana rangi ya Kijivu yenye nembo ya shule kwa ajili ya kushindia (**shamba dress, zinapatikana kwenye duka la shule).**

g) Soksi nyeupe.

h) Mkanda mweusi wa Ngozi wa kuvalia suruali.

### 2.2 *Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-*

i. Godoro jipya futi 2.5

ii. Shuka mbili rangi ya Blue, blanketi, chandarua rangi nyeupe**,** mto na foronya rangi ya Blue.

iii. Vyombo vya kulia chakula (sahani, bakuli, kikombe- vyote viwe vya udongo pamoja na kijiko.

iv. Ndoo mbili ndogo (lita 10) zenye mifuniko

v. Kwanja moja (PCM, PCB, CBG) na jembe **moja lenye mpini** (PCM, PCB, CBG, PGM na EGM)**.**

vi. Mfagio wa ndani (soft brooms), squeezer/mopa na mfagio wa nje (chelewa) (PGM na EGM).

vii. Ream za karatasi nne (4) aina ya A4 (double A) yaani mbili kwa kila mhula.

viii. Kadi ya bima ya afya ya NHIF. Kama hana bima, siku ya kuripoti njoo na Fedha kiasi cha shilingi elfu hamsini na mia nne tu (50,400/-) kwaajili ya kumkatia bima hiyo kwa mwaka mmoja. Hii ni lazima**.**

ix. Madaftari/Counter books (15) **quire 4**, vitabu (kama anavyo) na vifaa vingine kwa ajili ya masomo.

x. Dawa ya chooni lita tano (5)

xi. Brash ndogo moja (1) ya chooni.

xii. Dissecting kit kwa wanafunzi wanaosoma somo la **BIOLOGY**

xiii. Scientific calculator kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi na uchumi (PCM, PCB, CBG, PGM na EGM) File moja la kutunza kumbukumbu za mwanafunzi

xiv. Begi la kubebe la nguo/ sanduku la chuma (tranka)

xv. Rain boot

### 2.3 *Sheria na kanuni muhimu za shule.*

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria **Na. 25 ya mwaka 1978** na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria **Na 10 ya mwaka 1995.** Aidha, inazingatia miongozo yote iliyotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya WAZIRI MKUU – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa na maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

Mambo hayo ni pamoja na;

### 2.4 *Sheria na Kanuni za Shule.*

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani nan je ya shule kulingana na ratiba ya shule.

iii. Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku (Preparation) iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani nan je ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule. vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa. viii. viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote. ix. Kutunza mali za shule.

x. Ni marufuku kwa mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktarin; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

<u>MUHIMU:</u>

- ❖ Mwanfunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.
- ❖ Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.
- ❖ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule.
- ❖ Wageni wanao tambulika shuleni ni wale walioandikishwa kwenye faili la mwanafunzi na wanaruhusiwa kumtembelea mwanafunzi mara moja kwa muhula yaani (mara 2 kwa mwaka).
- ❖ Ni marufuku kuvaa kandambili wakati wa chakula katika Bwalo.

- ❖ Mwanafunzi ataruhusiwa kuja nyumbani kwa ajili ya msiba wa mama, baba, kaka ama dada tu na siyo mtu mwingine. Taarifa za misiba ziletwe moja kwa moja kwa Mkuu wa Shule siyo kwa mwanafunzi. Mwanafunzi hataruhusiwa iwapo utaratibu huu hautafuatwa.

## 2.5 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

**(i)** Wizi
**(ii)** Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
**(iii)** Kugoma na kuhamasisha mgomo
**(iv)** Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
**(v)** Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
**(vi)** Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
**(vii)** Uvutaji wa sigara.
**(viii)** Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa.
**(ix)** kusababisha mimba kwa mwanafunzi wa kike au mtu yeyote asiye mwanafunzi.
**(x)** Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
**(xi)** Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.
**(xii)** **Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule**
**(xiii)** Kudharau Bendera ya Taifa
**(xiv)** Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
**(xv)** Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.
**(xvi)** Kugomea adhabu halali.
**(xvii)** kunyoa nywele kwa mtindo usiokubalika **(xviii)** kufuga ndevu

## 3. <u>MICHANGO MBALIMBALI</u>

***A. SHULE ZA BWENI***

| S/N | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Mchango Wa Uendeshaji Wa Shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho Cha Shule | 5,000/= |
| JUMLA | | **80,000/=** |

MICHANGO HII ILIPWE KWENYE AKAUNTI YA SHULE.

BANKI: **NMB**
ACCOUNT NUMBER: **30510072867**
JINA LA ACCOUNT NI: **SIMIYU BOYS ELIMU YA KUJITEGEMEA**

**ANDIKA JINA LA MWANAFUNZI HUSIKA NA SI JINA LA MZAZI/MLEZI KWENYE PAY IN SLIP HUSIKA.**

**3. VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU**

a) Fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical Examination form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii atakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara atakaporipoti shuleni.

b) Fomu ya maelezo Binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.

c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatolewayo na shule.

d) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za Simu.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**



**JOHN MOSSES MAGOLANGA**

MKUU WA SHULE_

PICHA

**FOMU YA MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.**

Mimi________________________________ ambaye ni mwanafunzi niliyechaguliwa kujiunga na kidato cha Kwanza, tahasusi ya ____________ mwaka 2026 katika shule ya sekondari ya wavulana Simiyu, nakubali binafsi kujiunga na shule hii. Naahidi kuwa nitakuwa mwaminifu, mtiifu na mchapakazi wakati wote nikiwa mwanafunzi wa shule hii. Naahidi pia nitafuata sheria za shule na kuzingatia taratibu zote za shule, nitatunza mali zote za umma niwapo shuleni na naahidi kusoma kwa bidii zangu zote ili kuiletea sifa nzuri shule yangu na Taifa kwa ujumla.

Naahidi kushirikiana vyema na wanafunzi wenzangu katika masomo na shughuli zingine zote ndani ya eneo la shule, na pia nitaheshimu jumuiya nzima ya shule na kutoshiriki kwa namna yoyote ile katika mgomo, fujo na makosa ya jinai, na kwamba endapo nitaenda kinyume na mkataba huu nichukuliwe hatua za kinidhamu kulingana na sheria na taratibu za shule.

Saini ya mwanafunzi

Namba ya simu ya Baba_______________________

Namba ya simu ya Mama______________________

# HISTORIA NA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

**PICHA**

Jina la mwanafunzi: ----------------------------------------------

Majina ya wazazi (i) Baba-------------------------------------yuko hai/ amefariki(simu----------------)

(ii) Mama-----------------------------------yuko hai/amefariki (simu:---------------) Mahali wanapoishi wazazi:

Kijiji/mtaa----------------------------kata---------------------------------- wilaya---------------

-------------mkoa-------------------------- (kwa upande wa Baba)

Mama: kijiji/mtaa-------------------kata--------------------wilaya------------------mkoa-------------

Kabila la mwanafunzi-------------------------- dini na dhehebu----------------------------------------

Tarehe ya kuzaliwa---------------------- kijiji/mtaa------------------------- kata---------------------wilaya---------
---------------------mkoa-------------------------------Uraia--------------------------------

Shule ya msingi uliyosoma------------------------------------

Jina la mlezi (kama anatunzwa na mlezi) -----------------------------------------kijiji------------------mtaa-------
--------------kata--------------------wilaya---------------------mkoa---------------------------

Uhusiano na mlezi--------------------------- kazi ya mlezi------------------------------------------------

Namba ya simu ya mlezi: ------------------------------

Mbali na mlezi, mtu mwingine wa karibu ambae shule inaweza kufanya nae mawasiliano pindi upatapo matatizo------------------------------------------uhusiano-------------------------------------- Namba yake ya simu: -------------------------- mahali anapoishi------------------------------------- Kijiji/mtaa---------------------------------kata------------------------------wilaya----------------------

# OFISI YA WAZIRI MKUU

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## SHULE YA SEKONDARI YA WAVULANA SIMIYU

FOMU YA MKATABA KATI YA MZAZI WA MWANAFUNZI NA UONGOZI WA SHULE

Mimi-------------------------------------------ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi----------------------------- ------------------aliyechaguliwa kujiunga na kidato cha Kwanza mwaka 2026, naahidi kwamba nitampa mwanangu huduma zote zinazostahili kwa mwanafunzi wakati wote akiwa mwanafunzi wa shule ya sekondari ya wavulana Simiyu, na kwamba nitakuwa tayari kutimiza mambo yafuatayo:

a) Kumpa mwanangu huduma zinazostahili kama vile sare na mahitaji mengine ya muhimu.
b) Kushirikiana na walimu katika malezi bora ya mwanafunzi.
c) Kufika shuleni wakati wote ninapohitajika kutokana na utovu wa nidhamu utakaosababishwa na mwanangu na kuwa tayari kukubaliana na adhabu itakayotolewa na uongozi wa shule dhidi ya utovu wa nidhamu wa mwanangu.
d) Kufuatilia mara kwa mara maendeleo ya kitaaluma ya mwanangu wakati wote awapo mwanafunzi, na kuwa tayari kushirikiana na walimu katika kuboresha maendeleo ya mwanangu kitaaluma.
e) Nitakubaliana na adhabu yoyote itakayotolewa kwa mwanangu endapo ataenda kinyume na sheria za shule kama vile kugoma, kufanya fujo, kujihusisha na mapenzi, utoro, kutohudhuria darasani kwa makusudi, kupingana na sheria nyingine zote zilizo ainishwa katika fomu hii ya maelekezo.

**Mwisho; naahidi kuwa nitakuwa tayari kutekeleza kwa dhati mambo yote niliyoahidi kwa uongozi wa shule wakati wote mwanangu awapo mwanafunzi wa shule ya sekondari ya wavulana Simiyu**.

Saini ya Mzazi: ---------------------------

Namba za simu: -------------------------

# MEDICAL EXAMINATION FORM.

This form must be completed by Government Medical Officer.

**Student's full name.**___________________________________________

Age.__________________ sex.___________

☑ Blood test. ________________________________ Group _________

☑ Stool Examination_______________________________________________

☑ T.S Test_____________________________________________________ ☑

Asthma_____________________________________________________

☑ Eye Disorder___________________________________________________

☑ Ear Disorder___________________________________________________

☑ Nose Disorder__________________________________________________

☑ Anemia_______________________________________________________

☑ Chest________________________________________________________

☑ Operations_____________________________________________________

☑ Serious accidents_________________________________________________

☑ Any other infection disease_______________________________________ ☑

Pregnancy_______________________________________( Females only).

ADDITIONAL INFORMATION (Physical Impairment, chronic or Family disease e.t.c)

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

I certify that I have personally examined Mr. / miss__________________________

And found her/him

| fit | unfit |
|---|---|
| | |

to perform studies.

Signature ________________________________Designation_____________

Office rubber